

**KONGAMANO LA KUMALIZA UBAGUZI WA
AINA YOYOTE DHIDI YA WANAWAKE**

Wanawake 2000

Umoja wa Mataifa

Utangulizi

Kongamano la kumaliza ubaguzi wa aina yoyote dhidi ya wanawake lililokubaliwa na Baraza la Umoja wa Mataifa mwaka wa 1979 na kuelezwa kila mara kama sheria ya haki za wanawake Ulimwenguni. Sheria hiyo ina utangulizi na vifungu thelathini na hufafanua yale yanayochukuliwa kama ubaguzi dhidi ya wanawake na pia kuanzisha ajenda ya kushughulikia swala hili la ubaguzi.

Kongamano hilo lilifafanua ubaguzi dhidi ya wanawake kama, tofauti yoyote, kutengwa au kizuizi kwa sababu za kijinsia ambazo hauthiri hadhi na furaha ya wanawake bila kujali hali yao katika ndoa hasa usawa wao na ule wa wanaume unapolinganishwa kwa kuangalia haki za binadamu, uhuru wa kimsingi kupitia nyanja za kisiasa, kiuchumi, kijamii, kitamaduni na kiraia. Kwa kukubali Kongamano hilo, mataifa yalijitolea kuchukua jukumu la kusitisha ubaguzi wa aina yote dhidi ya wanawake kama vile:

- Kushirikisha maadili ya usawa wa wanaume na wanawake katika misingi ya kisheria na kupiga marufuku sheria zote za ubaguzi na kukubali zile zote zinazopinga ubaguzi dhidi ya wanawake;
- Kuanzisha mahakama na taasisi za umma za kuona kwamba wanawake wamelindwa na kuacha kubaguliwa;
- Kuangamizwa kwa vitendo vyote vya ubaguzi dhidi ya wanawake kupitia kwa watu au mashirika.

Kongamano hili linatoa nafasi ya kutambua usawa kati ya wanawake na wanaume na kuona kwamba wanawake wanafaulu kwa kupewa nafasi sawa na wanaume katika siasa, mambo ya taifa pia haki ya kupiga kura na kusimama katika uchaguzi, elimu, afya na kuajiriwa kazi. Vyama vya kitaifa vikubali kuchukua hatua mwafaka na sheria kufuatwa ili wanawake waweze kufurahia haki zao zote za kibinadamu na zile za kimsingi.

Kongamano hili ndiyo sheria ya kipekee ya haki za kibinadamu inayothibitisha haki za wanawake na kuingilia mila na desturi kama pingamizi kubwa kwa usawa wa kinjinsia na uhusiano wa kijamii. Hili ni thibitisho la haki za wanawake kuweza kumiliki, kubadilisha au kuhifadhi uraia wao na ule wa wana wao. Vyama vya kitaifa pia vikubali kuchukua hatua zifaazo dhidi ya dhuluma ya aina yoyote kama biashara ya kuwatumia wanawake kwa njia zisizofaa na kuwanyonya.

Nchi zilizoidhinisha au kukubali Kongamano zinawajibika kulilinda na kutekeleza kwa vitendo. Pia hujitolea kwa kuwasilisha ripoti za kitaifa mara moja kwa miaka mine kuhusiana na hatua walizochukua ili kukubaliana na matakwa ya Kongamano.

Kongamano hilo lilianzishwa tarehe 3 Septemba 1981 na kufikia tarehe 1 Novemba, 1999 wanachama walikuwa 165.

Itifaki ya Hiari kwa Kongamano

Tarehe 6 Oktoba, 1999, Baraza kuu kupitia kwa Itifaki ya Hiari lilikubali kuunga mkono Kongamano la kumaliza aina yoyote ya ubaguzi dhidi ya wanawake. Kupitia kwa mkutano wa Ulimwengu kuhusu Haki za binadamu (Vienna,1993) na mkutano wa nne wa wanawake ulimwenguni (Beijing,1995), nafasi ya kuanzisha haki ya maombi kulingana na Kongamano yaliwasilishwa.

Itifaki ya Hiari ina aina mbili za utaratibu. Utaratibu wa mawasiliano unaomruhusu mwanamke binafsi au kikundi cha wanawake kuwasilisha madai ya uonevu kwa kamati kulingana na Kongamano la Kumaliza ubaguzi dhidi ya wanawake.

Itifaki ya Hiari inahimiza kwamba kwa mawasiliano ya kibinafsi kuwasilisha na kuchunguzwa na kamati, lazima yafuate taratibu zilizowekwa kama kutafuta suluhisho nyumbani au kutoka kwa jamii. Itifaki ya Hiari pia huwa na tume inayofuata utaratibu unaosaidia kamati kuanzisha uchunguzi wa hali mbaya au hatua kwa hatua ya ukiukaji wa haki za wanawake. Katika hali hizi mbili, mataifa lazima yashirikiane. Itifaki ya Hiari inashirikisha ‘sheria ya kuamua kutoshiriki’ ambayo inaruhusu mataofa kujiondoa iwapo hawata kubaliana na utaratibu wa Kongamano.

Itifaki ya Hiari inatoa utaratibu usio na shaka.

Itifaki ya Hiari iliwasilishwa kwa kuwekwa sahihi na kukubaliwa tarehe 10 Desemba 1999 na itaanza kutekelezwa wakati mataifa kumi wanachama wa Kongamano wameikubali au kuiidhinisha. Baada ya kuidhinishwa, Itifaki ya Hiari itaweka Kongamano hili sawa na haki zingine za binadamu zilizoko ulimwenguni zilizo na nafasi ya mtu binafsi kuwasilisha malalamiko kama Kongamano la Ulimwenguni zilizo na nafasi ya mtu binafsi kuwasilisha malalamiko kama Kongamano la Ulimwengu la Haki ya Uraia na siasa, Kongamano la kuangamiza ubaguzi wa Kimbari na Kongamano dhidi ya mateso na aina nyingine ya ukatili, unyama au vitendo vyovyote vya kudunisha au kuadhibu.

Kongamano kuhusu kumaliza aina yoyote ya Ukatili dhidi ya Wanawake

Vyama vya Kitaifa katika kongamano la sasa,

Ifahamike kuwa mkataba wa Umoja wa Mataifa unathibitisha imani katika haki za binadamu za kimsingi, kwa heshima na thamani ya binadamu na haki na usawa wa wanawake na wanaume.

Ifahimike kuwa Azimio la Ulimwengu la haki za binadamu linathibitisha kanuni za ubaguzi zisizokubaliwa na kutangaza kuwa binadamu wote walizaliwa wakiwa huru na ni sawa kwa hali zote na wanastahili haki zote za kibidamu bila ubaguzi wa hali yoyote hata ule wa kijinsia.

Ifahamike kuwa Mataifa ya Ulimwengu yaliyoshiriki katika kongamano la haki za binadamu yana wajibu wa kuona kwamba wanaume na wanawake wana haki ya kufurahia uchumi, utamaduni, ushirikiano wa kijamii, uraia na haki ya kisiasa,

Ileweke kuwa kongamano la ulimwengu lilihitimishwa chini ya usimamizi wa Umoja wa Mataifa na mashirika maalum yanayoimarisha usawa wa wanaume na wanawake,

Ifahamike pia, kuwa makubaliano, maazimio na mapendekezo yaliyokubaliwa na Umoja wa Mataifa na mashirika maalum ili kuimarisha usawa na haki za wanaume na wanawake.

Ileweke kuwa, ingawa mengi yanafanywa lakini ubaguzi dhidi ya wanawake ungali unaendelea,

Ikumbukwe kuwa, ubaguzi dhidi ya wanawake unakiuka kanuni za usawa na heshima kwa binadamu ni pingamizi kwa wanawake kuweza kushiriki kikamilifu sawa na wanaume katika maswala ya kisiasa, kijamii, kiuchumi na kitamaduni katika nchi zao na kuzuia maendeleo ya jumua na jamii na kuzidisha ugumu wa wanawake kuweza kushiriki kikamilifu katika kuhudumia nchi zao na binadamu,

Ileweke kuwa, katika hali ya umaskini wanawake ndio walio na nafasi ndogo zaidi za kuweza kupata chakula, matibabu, elimu, mafunzo, nafasi za kazi na mahitaji mengine,

Ushawishi tosha kuwa kuimarishwa kwa sheria ya ulimwengu ya uchumi iliyoanzishwa kwa misingi ya usawa na haki itachangia sana katika kuimarisha usawa kati ya wanaume na wanawake,

Kusisitiza kuwa ufutiliaji mbali wa siasa ya ubaguzi wa rangi, hali zote za ubaguzi, ubaguzi wa kimbari, ukoloni, ukoloni mamboleo, uchokozi, uvamizi, umilikaji na uingiliaji katika maswala ya taifa na nchi nyingine ni muhimu ili wanaume na wanawake waweze kufurahia haki zao.

Kuthibitisha kuwa kuimarishwa kwa amani na usalama, ulimwengu, upungufu wa migogoro, ushirikiano kati ya mataifa bila kujali hali zao za kijamii na kiuchumi, upunguzaji wa silaha hasa zile za kitoradi chini ya udhibiti wa sheria ya Ulimwengu kuhusu haki, usawa na manufaa ya maafikiano kati ya nchi na kufahamu haki za watu walio chini ya ukoloni na uvamizi wa uhuru wao kutoka nje na pia heshima kwa uhuru wa taifa na mipaka yake kutaimarisha maendeleo na kuchangia kikamilifu katika shughuli za usawa kati ya wanawake na wanaume,

Ushawishi kuwa maendeleo kamili ya nchi, ustawi wa dunia na mpango wa amani unahitaji ushiriki kamili kutoka kwa wanawake wakipatiwa nafasi sawa na wanaume katika nyanja zote,

Zingatia mchango mkubwa uliofanyiwa na wanawake katika ustawi wa jamii na maendeleo ya jumuiya ambao mpaka sasa haujatambuliwa, swala nyeti la jamii la uzazi na wajibu wa kila mzazi katika familia na kwamba ulezi wa watoto unahitaji jukumu la wote kati ya wanaume na wanawake na jumuiya kwa ujumla,

Fahamu kwamba mabadiliko ya kitamaduni kuhusu jukumu la wanaume na wanawake katika jumuiya na jamii yanafaa kuwepo ili usawa kamili wa wanaume na wanawake upatikane,

Dhamira ya kutekeleza kanuni zilizopendekezwa katika Azimio la kumaliza ubaguzi wa aina yoyote dhidi ya wanawake na kwa sababu hiyo kukubali mbinu zinazohitajika ili kumaliza ubaguzi huo katika hali zote na waziwazi,

Makubaliano ni kama ifuatavyo:

Sehemu ya 1

Kifungu cha 1

Kwa kusudi la Kongamano la sasa, neno “ubaguzi dhidi ya wanawake” litakuwa na maana ya kutofautisha, kubagua au kuzuia kwa sababu za kimaumbile na kuleta athari za kuharibu au kuondoa kujulikana, kufurahia au kushiriki kwa wanawake kikamilifu katika shughuli za kisiasa, kiuchumi, kijamii, kitamaduni, kiraia au nyanya zingine zozote bila kujali hali yao ndoa bali usawa kati ya wanaume na wanawake, Haki za kibinadamu na haki zote za kimsingi.

Kifungu cha 2

Mataifa yana laani ubaguzi wa hali yoyote dhidi ya wanawake, kukubali kuendelea na shughuli ya kumaliza ubaguzi dhidi ya wanawake na kushughulika na:

- a) Kupamba kanuni za usawa wa wanaume na wanawake katika katiba zao za kitaifa au sheria zingine mwafaka ambazo hazijakubaliwa bado na kuona kwamba jambo hili linakamilika kupitia sheria na mbinu zilizopendekezwa na kukubalika;

- b) Kukubali sheria zifaazo na mbinu zingine pamoja na vikwazo mwafaka, kumaliza ubaguzi wa hali zote dhidi ya wanawake;
- c) Kuimarisha sheria za kulinda haki za wanawake sawa na wanaume kupitia kwa tume za kitaifa na taasisi za umma kuona kwamba wanawake wanalindwa dhidi ya vitendo vya ubaguzi;
- d) Kujizuia kujihusisha na vitendo au shughuli za ubaguzi dhidi ya wanawake na kuona kwamba viongozi wa umma na taasisi mbali mbali zitaimarisha wajibu huu;
- e) Kuchukua hatua zifaazo ili kumaliza ubaguzi dhidi ya wanawake utakaofanywa na mtu yeyote au shirika;
- f) Kuchukua hatua zifaazo pamoja kurekebisha au kukomesha sheria zilizoko, kanuni, mali na desturi ambazo zinaendeleza ubaguzi dhidi ya wanawake;
- g) Kubatilisha adhabu zote za kitaifa zinazotolewa na ambazo zinaendeleza ubaguzi dhidi ya wanawake.

Kifungu cha 3

Vyama vya kitaifa vitachukua hatua zifaazo katika nyanja ya kisiasa, kijamii, kiuchumi na kitamaduni zikiwemo sheria rasmi ili kuona kwamba uimarishaji wa maendeleo ya wanawake umefaulu kwa madhumuni ya kuwapa furaha ya uhuru kamili wa haki za binadamu na zile za kimsingi sawa na wanaume.

Kifungu cha 4

1. Vyama vya kitaifa kukubali hatua za muda zilizo na lengo la kuleta usawa kati ya wanaume na wanawake na zichukuliwe kuwa ni ubaguzi kama ilivyo katika Kongamano lakini zitashughulika madhara yanayotokana na ubaguzi unapoendelezwa. Hatua hizi zaweza kuachwa baada ya shabaha au kusudi kupatikana.
2. Vyama vya kitaifa kukubali hatua spesheli zikiwemo zile zilizo katika Kongamano la sasa lililo na shabaha ya kulinda uzazi na zisichukuliwe kuwa ni ubaguzi.

Kifungu cha 5

Vyama vya kitaifa vitachukua hatua hizi muhimu:

- a) Kurekebisha tabia za kijamii na kitamaduni za wanaume na wanawake ili kuangamiza ubaguzi mila na desturi hasa mawazo ya kuona watu wengine ni bora au duni wawe wake au waume au misimamo ya kijadi ya wanaume na wanawake.

- b) Kuona kwamba Elimu ya Kijamii inahusisha uelewaji vema wa likizo ya uzazi, kama jambo la kijamii na utambuzi wa kujua kwamba jukumu la ulezi wa watoto lazima lipewe umuhimu.

Kifungu cha 6

Vyama vya kitaifa vitachukua hatua zifaazo pamoja na sheria ili kuangamiza biashara ya wanawake hasa udunishaji wao kupitia kwa ukahaba.

SEHEMU YA II

Kifungu cha 7

Vyama vya kitaifa vitachukua hatua zifaazo ili kuangamiza ubaguzi dhidi ya wanawake katika siasa na maisha ya kawaida nchini hasa kuona kwamba wanawake wanapata usawa na haki zifuatazo:

- a) Kuweza kupiga kura na kushiriki katika kura za maoni, pia kuweza kusimama katika uchaguzi wowote ule.
- b) Kuweza kushiriki kikamilifu katika uanzishaji wa sera za kiserikali na kutawala katika nyanja zote za serikali.
- c) Kushiriki katika mashirika yasiyo ya kiserikali na yale yanayohusika na shughuli za umma na siasa za nchi.

Kifungu cha 8

Vyama vya kitaifa vitachukua hatua zifaazo kuona kwamba wanawake wana usawa na wanaume bila ubaguzi, wapewe nafasi ya kuiwakilisha serikali yao katika mikutano ya kimataifa na kushiriki katika shughuli au ajira za kimataifa.

Kifungu cha 9

1. Vyama vya kitaifa vitawapa wanawake haki sawa kama wanaume ili waweze kufanya mabadiliko ya kupata, kubadilisha au kuhifadhi uraia wao. Yafaa kuhakikisha kuwa kuolewa na mgeni au mume kuamua kubadilisha uraia wake wakati wa ndoa kamwe kusimlamishe mwanamke kubadili uraia wake au kumfanya kukosa uraia au kumlazimisha kuchukua uraia wa mumewe.
2. Vyama vya kitaifa vitawapa wanawake usawa kama wanaume na kuzingatia uraia wa wana wao.

SEHEMU YA III

Kifungu cha 10

Vyama vya Mataifa vitachukua hatua zifaazo kuangamiza ubaguzi dhidi ya wanawake ili kuwahakikishia haki sawa na wanaume katika uwanja wa elimu na katika misingi ya usawa wa wanaume na wanawake:

- a) Masharti sawa ya kikazi na ushauri wa kitaalamu wa kuweza kupata mafunzo na uwezekano wa kupata stahahada au diploma katika vyuo vya elimu vya aina mbalimbali mashambani na pia mijini; Usawa huu utahakikishwa katika shule za Chekechea, za kawaida, vyuo vya kazi na ufundi pia mafunzo ya taaluma zote;
- b) Nafasi ya kufunzwa kwa mitaala sawa, kufanya mitihani hiyo hiyo, walimu walio na vyeti vya kuhitimu na viwango sawa, shule na vifaa vikiwa vya hali moja pia;
- c) Kuangamizwa kwa fikira za kimsingi za jukumu la wanaume na wanawake wa viwango mbalimbali na miundo mabalimbali ya elimu kwa kuhimiza elimu kwa jinsiya zote na aina zingine za elimu ambazo zitasaidia kufanikisha lengo hili hasa kwa kufanya marudio ya vitabu na mipango ya shule na mabadiliko ya njia za kufundisha;
- d) Nafasi sawa ile ufanisi uweze kupatikana kupitia kwa utaalumu na misaada ya masomo;
- e) Nafasi sawa ili mipango ya elimu iendelee pamoja na masomo kwa watu wazima na mipango ya kumaliza kutojua kusoma hasa ile itakayopunguza tofauti za elimu zilizoko kati ya wanaume na wanawake kwa haraka.
- f) Kupunguza idadi ya wanafunzi wa kike wanaoacha shule na kuwa na mipango ya kuwafaa wasichana na wanawake hao;
- g) Nafasi zitolewe ili kushiriki kikamilifu katika mashindano ya riadha na Elimu ya mazoezi ya viungo au kwata;
- h) Nafasi ya habari maalum za elimu ili kusaidia na kuona kwamba afya na hali ya jamii ni bora pamoja na kuwapa ushauri juu ya mipango ya uzazi.

Kifungu cha 11

- 1) Vyama vya Kitaifa vitachukua hatua zifaazo kuangamiza ubaguzi dhidi ya wanawake katika nyanja za ajira ili kuona kwamba kuna usawa wa wanaume na wanawake, haki sawa hasa:
 - a) Haki ya kufanya kama haki isiyoondolewa kwa binadamu yeyote;

- b) Haki ya nafasi sawa za na utumiaji wa kigezo sawa wakati wa mchujo wa kazi hiyo;
 - c) Haki ya kufanya uchaguzi wa kazi au utaalamu, haki ya kupandishwa cheo, usalama kazini na kupewa faida ya huduma, na haki ya kupata mafunzo ya kiufundi, uanagenzi, mafunzo ya juu ya kiufundi na yale ya mara kwa mara;

 - d) Haki ya kupata tuzo sawa pamoja na faida, kutendewa ya kazi heshima sawa bila kuzingatia aina ya kazi na pia usawa wa tathmini ya kazi;
 - e) Haki ya mapato ya uzeeni hasa wakati wa kustaafu, ugonjwa, unaposhindwa kufanya kazi, kuishiwa na nguvu, uzee na kizuizi cha kutofanya kazi na pia haki ya kulipwa pesa za likizo;
 - f) Haki ya ulinzi wa kiafya na usalama kazini ili kulinda uzalishaji.
- 2) Ili kuzuia ubaguzi dhidi ya wanawake katika ndoa au wakati wa uzazi na kuona kwamba wamepewa haki, vyama vya Kitaifa vitachukua hatua zifaazo:
- a) Kupinga kuweco kwa vikwazo, kufukuzwa kwa sababu ya kuwa mja mzito au kuchukua likizo ya uzazi kufukuzwa kwa sababu ya hali ya ndoa;
 - b) Kuwe na likizo ya uzazi pamoja na malipo au malipo ya kijamii bila kuachishwa kazi, cheo au kunyimwa marupurupu;
 - c) Kuhimiza kuwepo kwa mifumo ifaayo ya huduma za kijamii ili wazazi waweze kufanya kazi, kuhudumia jamii zao na kushiriki katika maisha ya kila siku hasa kwa kuimarisha na kuendeleza sehemu za kuwatunzia watoto;
 - d) Kutoa ulinzi spesheli kwa wanawake hasa wakiwa waja wazito na hasa wanapoendelea kufanya kazi zile zinazowaletea madhara.
- 3) Sheria ya Ulinzi kuhusu mambo yaliyojadiliwa katika kifungu hiki yatakuwa yakirejelewa kila mara kulingana na misingi ya kisayansi au kiteknolojia ili kubatilisha au kurekebisha ipasavyo.

Kifungu cha 12

- 1) Vyama vya kitaifa vitachukua hatua zote zifaazo ili kuangamiza ubaguzi dhidi ya wanawake katika nyanja ya afya ili kuona kwamba kuna usawa wa wanaume na wanawake katika huduma za kiafya zikiwemo zile za upangaji uzazi.
- 2) Licha ya huduma itolewayo katika kifungu cha 1, Vyama vya kitaifa vafaa kuona kwamba wanawake wamepewa huduma zinazohusiana na uja uzito, wanapojifungua na waweze kupewa huduma za bure zinapohitajika, lishe bora wanapokuwa waja wazito na wanaponyonyesha.

Kifungu cha 13

Vyama vya Kitaifa vichukue hatua zote zifaazo ili kuangamiza ubaguzi dhidi ya wanawake katika nyanja ya kiuchumi na kijamii ili kuona kwamba kuna usawa wa wanawake na wanaume na kuwa na haki sawa hasa:

- a) haki ya manufaa ya jamii;
- b) Haki ya kupata mikopo ya benki, kuweka rehani na misaada mingine ya kifedha au mikopo;
- c) Haki ya kushiriki katika shughuli za michezo, burudani na kitamaduni.

Kifungu cha 14

- 1) Vyama vya kitaifa vitashughulikia shida zinazowakumba wanawake wa mashambani na mchango wao katika sekta ya kiuchumi wa kuinua familia zao, kazi wanazofanya bila malipo na hatua zifaazo kuchukuliwa kulingana na Kongamano ili kuwalinda wanawake wa mashambani.
- 2) Vyama vya kitaifa vichukue hatua kuangamiza ubaguzi dhidi ya wanawake wa mashambani ili kuona kwamba kuna usawa wa wanaume na wanawake na waweze kushiriki na kufaidika kupitia kwa miradi ya maendeleo ya huko mashambani na hasa kuona kwamba wanawake wana haki zifuatazo:
 - a) Kushiriki katika ufafanuzi na uimarishaji wa mipango ya kimaendeleo katika viwango vyote;
 - b) Kupata matibabu, kuelimishwa, kupata huduma ya ushauri na mpango wa uzazi;
 - c) Kupata msaada wa moja kwa moja kutoka kwa mipango ya huduma za jamii;
 - d) Kupata mafunzo ya elimu ya aina mbalimbali ili kuondoa ujinga, kupata manufaa kwa jumuiya na ongezeko la huduma la kuongeza maarifa ya kiufundi;
 - e) Kuanzisha makundi ya kujisaidia wenyewe na vyama vya ushirika ili kupata nafasi sawa za kichumi kupitia kwa ajira au kujiandika kazi za kibinafsi;
 - f) Kushiriki katika shughuli za kijamii;
 - g) Kupata mikopo na misaada ya fedha katika kilimo, elimu ya soko, ufundi ufaao na usawa katika maswala ya ardhi, umilikaji ardhi na shughuli ya kutoa makao mapya;
 - h) Kufurahia hali ya makao hasa nyumba, umeme na utoaji maji, mawasiliano na usafiri.

SEHEMU YA IV

Kifungu cha 15

- 1) Vyama vya kitaifa vitawapa wanawake usawa sawa na wanaume kulingana na sheria.
- 2) Vyama kitaifa vitawapa wanawake ulinzi wa kisheria katika mambo ya kijamii sawa na wanaume na nafasi sawa ya kuutekeleza. Hasa kuwapa wanawake haki sawa za kukamilisha kandarasi na kusimamia mali pia kuthaminiwa katika shughuli hii kortini na kwenye baraza.
- 3) Vyama vya kitaifa kukubali kuwa kandarasi zote na shughuli zote za kibinafsi zinazofuata sheria lakini zinazuia wanawake kujiendeleza zitachukuliwa kuwa hazifai.
- 4) Vyama vya kitaifa vitawapa wanaume na wanawake haki sawa kulingana na sheria inayoruhusu watu kwenda kokote watakako na uhuru wa kuchagua nyumba na makazi yao.

Kifungu cha 16

- 1) Vyama vya kitaifa vitachukua hatua zifaazo ili kuangamiza ubaguzi dhidi ya wanawake katika maswala yote ya ndoa na uhusiano wa kijamii hasa kuona kwamba kuna usawa kati ya wanaume na wanawake.
 - a) Haki sawa ya kuwa katika ndoa;
 - b) Haki ya kuchagua mwenzi wa ndoa kwa hiari na kuolewa bila kulazimishwa;
 - c) Haki na wajibu sawa katika ndoa na talaka;
 - d) Haki na wajibu sawa kama wazazi kwa mambo yanayohusu watoto licha ya nafasi na kwa kila hali mahitaji ya watoto yawe muhimu;
 - e) Haki hizo zitumiwe kufanya uamuzi wa idadi ya watoto watakozaliwa, kupanga wakati watakozaliwa na kuwa na habari, elimu na jinsi ya kushughulika ili haki hizo zipatikane;
 - f) Haki hizo na wajibu wa ulezi, udhamini na upangaji wa watoto au Taasisi zinazoimarisha haki hizo kwa kufuata sheria za Taifa na kuweka mahitaji ya watoto mbele;
 - g) Haki za kibinafsi za bwana na bibi zikiwemo haki ya kuchagua jina la familia, ajira na kazi;
 - h) Haki sawa kwa wote walioana kwa kuheshimu umilikaji, usimamizi, utawala, furaha na utoaji wa mali bure au kwa kununua;

- 2) Kuchumbiwa na kuolewa kwa mtoto hakutaathiriwa na sheria na kila kitu kitafanywa ili kufafanua umri wa wastani wa kufunga ndoa na usajili wa ndoa katika ofisi ya msajili wa ndoa kuwa lazima.

SEHEMU YA V

Kifungu cha 17

- 1) Kwa madhumuni ya kutaka kujua maendeleo yaliyofanywa katika utekelezaji wa Kongamano la sasa, kamati itaimarishwa ili kuangamiza ubaguzi dhidi ya wanawake (Itajulikana kama kamati) itahusisha wanachama kumi na nane mwanzoni na baada ya uidhinishaji wa Kongamano la vyama thelathini na tano vya kitaifa kutakuwa na wataalam ishirini na watatu wenye heshima na ujuzi katika nyanja iliyoshughulikiwa na Kongamano. Wataalam hawa watateuliwa na vyama vya kitaifa kutoka kwa mataifa yao na watatoa huduma za kibinafsi, huku usambazaji na maeneo ya kule watokako ukizingatiwa ili ustaaraabu wa hali zote na mifumo ya sheria pia kupewa kipa umbele.
- 2) Wanachama wa kamati watachaguliwa kwa kura ya siri kutokana na majina yaliyopendekezwa na vyama vya kitaifa. Kila chama cha kitaifa kinaweza kuteua mtu mmoja kati ya wananchi wake.
- 3) Uchaguzi wa kwanza utafanywa siku sita baada ya kuanzishwa kwa Kongamano la sasa. Miezi mitatu kabla ya siku ya uchaguzi, Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa ataandika barua kwa vyama vya kitaifa akiwashauri kutuma maombi yao ya uteuzi kabla ya muda wa miezi miwili. Katibu mkuu pia atatarisha majina ya wale walioteuliwa kwa njia ya alfabeti na kuonyesha vyama vya kitaifa vilivyoteua mjumbe na kuwasilisha jina kwa vyama hivyo.
- 4) Uchaguzi wa wanachama utafanywa wakati wa mkutano wa vyama vya kitaifa utakaoitwa na katibu mkuu wa Umoja wa Mataifa katika makao kuu. Katika mkutano huo thuluthi mbili za wanachama zitawezesha kuendelea na mkutano na wale watakaochaguliwa kwa kamati watakuwa watu walioteuliwa na kupata kura nyingi zaidi kutoka kwa wawakilishi wa vyama vya kitaifa waliohudhuria kikao.
- 5) Wanachama hao wa kamati watahudumu kwa muda wa miaka minne. Kipindi cha kuhudumu cha wanachama tisa waliochaguliwa katika uchaguzi wa kwanza kitaisha baada ya miaka miwili; Mwenyekiti wa kamati atawachagua hao tena kwa haraka kwa kura ya bahati nasibu baada ya uchaguzi wa kwanza.

- 6) Uchaguzi wa wanachama wengine watano utafanywa kulingana na aya ya 2,3 na 4 ya kifungu hiki kwa kufuata uthibitisho au uidhinishaji wa thelathini na tano wa Kongamano. Kipindi cha kuhudumu cha wanachama wengine wawili waliochaguliwa kitaisha baada ya miaka miwili. Majina yao yatakuwa yamechaguliwa kwa bahati nasibu na mwenyekiti wa kamati.
- 7) Kwa kujaza nafasi za muda, chama cha kitaifa kilicho na mtaalam aliyeacha kufanya kazi kama mwanakamati kinaweza kuchagua mtaalamu mwingine kati ya wananchi wake na kungoja idhini kutoka kwa kamati.
- 8) Idhini ikitoka kwa Baraza kuu la Umoja wa Mataifa wanachama wa kamati wanaweza kupewa mshahara kulingana na makubaliano ya Baraza na baada ya kuangalia umuhimu wa kamati na jukumu lake.
- 9) Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa atatoa wafanya kazi na vifaa vya utumishi ili kuendeleza utekelezaji wa kazi nzuri.

Kifungu cha 18

- 1) Vyama vya kitaifa vinapaswa kuwasilisha ripoti kwa Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa kuhusu hatua zilizokubaliwa za kisheria, kimahakama na kiutawala ili kuimarisha maswala ya Kongamano la sasa na maendeleo yaliyofanywa kama ifuatavyo:
 - a) Kati ya mwaka mmoja baada ya taifa kujiunga na
 - b) Baadaye kwa miaka minne hivi na zaidi kamati ikihitaji kufanya uchunguzi.
- 2) Ripoti zaweza kugusia shida na mambo yanayokumba uimarishaji na utekelezaji wa Kongamano la sasa.

Kifungu cha 19

- 1) Kamati itakubali sheria zake za utekelezaji wa shughuli.
- 2) Kamati itawateua maafisa wake kwa kipindi cha miaka miwili.

Kifungu cha 20

- 1) Kamati itakutana kwa kawaida kwa muda usiozidi wiki mbili kwa mwaka ili kuchunguza ripoti zilizowasilishwa kulingana na kifungu cha 18 cha Kongamano la sasa
- 2) Vikao vya kamati kwa kawaida vitafanyika katika Makao Makuu ya Umoja wa Mataifa au mahali kwengine kokote kamati inakoamua.

Kifungu cha 21

- 1) Kamati itapiga ripoti kwa Baraza kuu la Umoja wa Mataifa kupitia kwa Baraza la Uchumi na Kijamii kuhusu shughuli zake na itaweza kufanya mapendekezo na kutoa maoni ya ripoti hizo na maelezo yaliyopokewa kutoka kwa vyama vya kitaifa.

- 2) Katibu Mkuu atawasilisha ripoti hizo kwa kamati ya shirika juu ya hali ya wanawake.

Kifungu cha 22

Mashirika spesheli au maalum yana haki ya kupata wawakilishi katika uimarishaji wa Kongamano la sasa kama mojawapo ya shughuli zao. Kamati yaweza kualika mashirika hayo spesheli au maalum kuwasilisha ripoti za uimarishaji wa Azimio hasa katika shughuli wanazoshughulikia.

SEHEMU YA VI

Kifungu cha 23

Hamna chochote katika Kongamano kinachoweza kuathiri uimarishaji ufaao kuhusu usawa kati ya wanaume na wanawake ambao unapatikana kwenye:

- a) Sheria za Chama cha kitaifa; au
- b) Katika Kongamano lolote la kimataifa, sheria au makubaliano yaliyoidhinishwa na Taifa.

Kifungu cha 24

Vyama vya kitaifa vitashughulikia hatua zote za kitaifa zinazochangia kupata haki zilizokubaliwa katika Kongamano la sasa.

Kifungu cha 25

- 1) Kongamano la sasa litakuwa tayari kukubali sahihi za mataifa yote
- 2) Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa ndiye anayehusika na uhifadhi wa Azimio la sasa.
- 3) Kongamano la sasa linahitaji marekebish., Vifaa vya uidhinishaji vitahifadhiwa na Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa.
- 4) Kongamano la sasa litakuwa huru kukubaliwa na taifa lolote. Makubaliano yataimarishwa kwa kuweka vifaa vya idhini vitahifadhiwa kwa Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa.

Kifungu cha 26

- 1) Ombi la kufanyia marekebisho kwa Kongamano la sasa laweza kufanywa wakati wowote na chama chochote cha kitaifa kwa njia ya kujulisha kwa kumwandikia Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa.
- 2) Baraza kuu la Umoja wa Mataifa litatoa uamuzi na hatua zipaswazo kufuata kulingana na ombi hilo.

Kifungu cha 27

- 1) Azimio la sasa litakubalika siku ya thelathini baada ya kuhifadhiwa na Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa katika hatua ishirini katika shughuli za uidhinishaji.
- 2) Kwa kila taifa linaloidhinisha Kongamano la sasa au kulikubali baada ya kuhifadhiwa kama hatua ya ishirini ya uidhinishaji au makubaliano. Kongamano litaanza kukubaliwa katika siku ya thelathini baada ya tarehe ya kuidhinishwa..

Kifungu cha 28

- 1) Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa atapokea na kueneza makala ya shaka yaliyotolewa na Mataifa wakati wa marekebisho au kuidhinisha.
- 2) Usetiri unaolingana na kusudi la Kongamano la sasa hautakubaliwa.
- 3) Usetiri waweza kuondolewa wakati wowote mradi Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa ajulishe ili ajulishe vyama vya Kitaifa. Ilani hiyo itakubaliwa tarehe itakayopokolewa.

Kifungu cha 29

- 1) Kutoelewana kokote kati ya vyama vya kitaifa kuhusu tafsiri au matumizi ya Kongamano la sasa ambako hakutakuwa kumesuluhishwa kupitia kwa majadiliano kutawasilishwa kwa mpatanishi ikiwa upande wowote ule utaomba usaidizi. Ikiwa mzozo huu hautatuliwa baada ya miezi sita baada ya ombi la utatuzi kuwasilishwa, upande wowote unaohusika unaweza kuwasilisha ugomvi huo katika mahakama kuu ya ulimwengu kulingana na sheria za mahakama.
- 2) Kila chama cha kitaifa kina uhuru wa kujiondoa kwenye masharti ya kifungu cha 1 cha makala haya kabla ya uidhinishaji au utiaji sahihi wa Kongamano. Vyama vingine vya Kitaifa pia havitalazimishwa kufuata aya ya 1 ya kifungu hiki hata kama upande huo utakuwa umewasilisha ombi lake.
- 3) Chama chochote cha Kitaifa ambacho kitakuwa kimewasilisha ombi la usetiri kulingana na aya ya 2 ya kifungu hiki kinaweza kuondoa ombi lake wakati wowote kupitia kwa Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa.

Kifungu cha 30

Makala ya Kongamano la sasa katika lugha ya kiarabu, kiingereza, kifaransa, kirusi na kihspania ambayo ni ya asili yatawekwa kwa Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa.

HITIMISHO

ITIFAKI YA HIARI KWA KONGAMANO LA KUANGAMIZA UKATILI WA AINA YOYOTE DHIDI YA WANAWAKE

Vyama vya kitaifa katika Itifaki ya sasa.

Ifahamike kwamba mkataba wa Umoja wa Mataifa unathibitisha imani katika haki za kimsingi, heshima na thamani ya mwanadamu na haki na usawa wa wanaume na wanawake,

Ifahamike pia kwamba Azimio la Ulimwengu la Haki za binadamu linasema kuwa binadamu wote ni sawa katika heshima na haki na kila mtu anastahili uhuru wa hali zote bila ubaguzi wa aina yoyote na bila ubaguzi wa kijinsia,

Ikumbukwe kuwa kongamano la Ulimwengu kuhusu haki za binadamu, mashirika mengine ya haki za binadamu yamepiga marufu ubaguzi kwa misingi ya kijinsia,

Ikumbukwe pia kwamba kongamano la kuangamiza ubaguzi wa aina yoyote dhidi ya wanawake (“kongamano”), ambapo vyama vya kitaifa vililaani ubaguzi wa aina yoyote dhidi ya wanawake na kukubali kuendeleza harakati za kuangamiza ubaguzi dhidi ya wanawake,

Kwa Kuthibitisha ari yao na kuona kuwa wanawake wamefurahia haki zote hata uhuru wa kimsingi na kuchukua hatua zifaazo ili kuzuia uvunjaji wa haki na uhuru huu kama ifuatavyo:

Kifungu cha 1

Chama cha kitaifa kitakachoshiriki katika Itifaki ya sasa (“Chama cha kitaifa”) kitambue uhodari wa Kamati ya kuangamiza ubaguzi dhidi ya wanawake, (“Kamati”) kupotea na kushughulikia mawasiliano yaliyowasilishwa kulingana na kifungu cha 2.

Kifungu cha 2

Mawasiliano yanaweza kuwasilishwa na watu binafsi au kwa niaba yao au kwa niaba ya kikundi cha watu chini ya mamlaka ya Chama cha Kitaifa na kwa wale wanaodai kuwa wahasiriwa wa kuvunjiwa haki kama sheria ilivyo katika Kongamano. Mawasiliano yanapowasilishwa kwa niaba ya watu au kundi la watu, hii iwe kwa hiari yao au sivyo anayewasilisha kwa niaba yao atoe kibali kuthibitisha kuteuliwa kwake.

Kifungu cha 3

Mawasiliano yatawasilishwa katika maandishi na majina kuwekwa wazi. Hamna mawasiliano yatakayopokelewa na kamati ikiwa Chama cha Kitaifa katika Kongamano sio mwanachama wa Itifaki ya sasa.

Kifungu cha 4

- 1) Kamati haitakubali mawasiliano hadi ihakikishe kuwa suluhisho la kinyumbani limeshughulikiwa vya kutosha au mapendekezo hayatafaa.
- 2) Kamati yaweza kuzuia mawasiliano yasipokelewe wakati ambapo:
 - a) Jambo hilo hilo liwe limekwishajadiliwa chini ya sheria za uchunguzi za Kilimwengu;
 - b) Ikiwa hayaambatani na makubaliano ya Azimio;
 - c) Ikiwa haikuanzishwa au kuelezwa vema;
 - d) Ikiwa sheria za haki ya kuwasilisha mawasiliano imekiukwa;

- e) Matendo ambayo yanahusu mawasiliano yawe yamefanyika kabla ya Itifaki ya Chama cha Kitaifa kukubaliwa au sivyo matendo yaliendelea baada ya tarehe hiyo.

Kifungu cha 5

- 1) Wakati wowote baada ya mawasiliano kupokelewa na kabla ya uamuzi kufikiwa kamati yaweza kuwasilisha kwa chama cha kitaifa na kuchukua hatua zifaazo ili kuzuia hasara kwa mhasiriwa au wahasiriwa wa ukiukaji huo.
- 2) Pale ambapo Kamati yaweza kutumia hadhari kwa kuzingatia aya ya 1 ya kifungu hiki, hii haimanishi kwamba ni uamuzi wa ukubalifu au kulingana na ustahilifu wa mawasiliano.

Kifungu cha 6

- 1) Ikiwa kamati itaona kuwa mawasiliano hayafai bila idhini kutoka kwa chama cha kitaifa kinachohusika na ikiwa mtu au watu binafsi watadhihirisha asili yao kwa chama cha kitaifa. Kamati yaweza kuleta mawasiliano yaliyowasilishwa kwa kuzingatia siri ya Kongamano la sasa na kuwasilisha kwa chama cha Kitaifa kinachohusika.
- 2) Chama cha Kitaifa kinapaswa kuwasilisha maelezo yaliyoandikwa au habari inayofafanua swala hili na kutoa suluhisho kutoka kwa Chama cha Kitaifa kama lipo.

Kifungu cha 7

- 1) Kamati itaangalia mawasiliano itakayopokea kulingana na Itifaki ya sasa na kushughulikia mambo yote kwa niaba ya mtu binafsi au kundi la watu na kwa Chama cha Kitaifa kinachohusika bora tu habari hiyo iwe imewasilishwa kwa vyama vinavyohusika.
- 2) Kamati itaandaa mikutano ya faragha inapochunguza mawasiliano kulingana na Itifaki ya sasa.
- 3) Baada ya uchunguzi, kamati itawasilisha maoni yao juu ya mawasiliano pamoja na mapendekezo ikiwa yatakuwepo kwa vyama vinavyohusika.
- 4) Chama cha Kitaifa kitawasilisha maoni ya Kamati pamoja na mapendekezo ikiwa yatakuwepo na kuwasilisha kwa kamati kati ya miezi sita na kutoa jibu lililoandaliwa pamoja na habari kuhusu hatua zilizochukuliwa kulingana na maoni na mapendekezo ya kamati.
- 5) Kamati yaweza kualika Chama cha Kitaifa ili kiwasilishe habari zaidi juu ya hatua zilizochukuliwa kama jibu kwa mawazo au maoni ikiwa yapo, pamoja na mtazamo mwafaka wa kamati na ripoti za Chama cha Kitaifa kulingana na kifungu cha 18 cha Kongamano.

Kifungu cha 8

- 1) Ikiwa kamati itapokea habari kamili zinazoonyesha ukiukaji wa sheria za Chama cha Kitaifa kulingana na Kongamano, basi kamati itaalika Chama hicho cha kitaifa na kuagiza ushirikiano wakati wa uchunguzi na kuwasilisha maoni kulingana na habari zinazohusika.
- 2) Kulingana na maoni ambayo yatakuwa yamewasilishwa na Chama cha Kitaifa husika pamoja na habari kamili zitakazokuwa zimepokewa, kamati itaweza kuteua mmoja kati ya wanachama wake kufanya uchunguzi na kisha kutoa habari au ripoti kwa kamati.

Tume hiyo ya uchunguzi yaweza kuzuru sehemu hiyo ikiwa itataka kufanya hivyo mradi kuwe na idhini kutoka kwa Chama cha Kitaifa.

- 3) Baada ya kuchunguza matokeo ya tume hiyo, kamati itawasilisha matokeo hayo kwa Chama cha Kitaifa kinachohusika pamoja na maoni na mapendekezo.
- 4) Chama cha Kitaifa kinachohusika kinapaswa kuwasilisha matokeo na mapendekezo kati ya miezi sita baada ya kuyapokea kutoka kwa kamati na kuwasilisha yote hayo kwa kamati.
- 5) Tume hiyo itaendesha shughuli zake kwa faragha na ushirikiano kutoka kwa Chama cha Kitaifa utapendekezwa wakati wote wa uchunguzi.

Kifungu cha 9

- 1) Kamati yaweza kukaribisha Chama cha Kitaifa husika kuwasilisha katika ripoti yake hatua zozote zilizochukuliwa kulingana na kifungu cha 18 cha Kongamano na maelezo zaidi yatolewe kwa tume kulingana na kifungu cha 8 cha Itifaki ya sasa.
- 2) Kamati yaweza kukaribisha Chama cha Kitaifa husika ikiwa ni muhimu baada ya muda wa miezi sita uliotajwa katika kifungu cha 8:4 na pia kutoa habari za hatua zilizochukuliwa kulingana na tume hiyo.

Kifungu cha 10

- 1) Kila chama cha Kitaifa kina uhuru wa kusema hadharani wakati wa kutia sahihi au kuidhinisha kuwa hakitambui uwezo wa kamati kama ilivyo katika kifungu cha 8 au 9.
- 2) Chama chochote cha Kitaifa kinapotangaza kulingana na aya ya 1 ya kifungu cha sasa kinaweza pia kufutiwa mbali msimamo huu kwa kutoa taarifa kwa Katibu Mkuu.

Kifungu cha 11

Chama cha Kitaifa kinaweza kuchukua hatua zote zinazostahili ili kuona kwamba watu chini ya milki yake hawaathiriwi na maonevu au tishio la aina yoyote kwa sababu ya kuwasiliana na kamati inayoshughulikia Itifaki ya sasa.

Kifungu cha 12

Kamati itaweka pamoja ripoti yake ya mwaka kulingana na kifungu cha 21 cha Kongamano la muhtasari wa shughuli zake zote chini ya Itifaki ya sasa.

Kifungu cha 13

Kila chama cha kitaifa kitachukua jukumu la kueneza habari juu Kongamano na Itifaki ya sasa na kuona kwamba habari hizi zimeelewekwa na kufahamika, maoni na mapendekezo ya kamati hasa mambo yanayohusu Chama cha Kitaifa pia kufahamika.

Kifungu cha 14

Kamati itakuwa na sheria zake za kufuata inaposhughulikia kazi iliyopewa na itifaki ya sasa.

Kifungu cha 15

- 1) Itifaki ya sasa itakuwa wazi kuwekwa sahihi kuweka na taifa lolote lililotia sahihi, kuidhinisha au kukubali Kongamano.

- 2) Itifaki ya sasa itakuwa wazi kuidhinishwa na taifa lolote lililokubali au kuidhinisha Kongamano. Vifaa vya uidhinishaji au makubaliano vitakuwa chini ya uangalizi wa Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa.
- 3) Itifaki ya sasa itakuwa wazi kuidhinishwa na taifa lolote ambalo limekubali au kuidhinisha Kongamano.
- 4) Idhinisho litaathiriwa na uwekaji wa kifaa cha idhinisho kwa Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa.

Kifungu cha 16

- 1) Itifaki ya sasa itaanza kutumika miezi mitatu baada ya tarehe ya uwekaji wa kifaa cha maidhinisho kwa Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa na kifaa cha Kumi cha maidhinisho au makubaliano.
- 2) Kwa kila taifa linalokubali Itifaki ya sasa au kuidhinisha baada ya kuanza kutumika, Itifaki ya sasa itaanza pia kutumika miezi mitatu baada ya tarehe ya uwekaji wa kifaa cha makubaliano au Idhinisho.

Kifungu cha 17

Hakuna shaka itakayoruhusiwa kwa Itifaki ya sasa.

Kifungu cha 18

- 1) Chama chochote cha Itifaki chaweza kupendekeza marekebisho kwa Itifaki ya sasa na kuwasilisha kwa Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa. Katibu Mkuu atawasilisha marekebisho yoyote yaliyopendekezwa kwa Vyama vya Kitaifa na ombi la kumjulisha ikiwa watapendelea kongamano la vyama vya kitaifa kwa madhumuni ya kuchunguza na kipigia kura marekebisho. Ikitokea kuwa thuluthi moja ya wanachama wa Kitaifa watapendelea kuwa na Kongamano, Katibu Mkuu ataita mkutano kulingana na sheria za Umoja wa Mataifa. Pendekezo lolote litakalokubaliwa na wengi wa wanachama wa Vyama vya Kitaifa watakaoshiriki katika kura litawasilishwa kwa Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa ili likubaliwe au kupitishwa.
- 2) Mapendekezo yoyote yataanza kutumika yanaokukubaliwa na Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa na pia kukubaliwa na thuluthi tatu ya wanachama wa vyama vya Kitaifa katika Itifaki ya sasa kulingana na katiba zao.
- 3) Mapendekezo yanapotumika, yatakuwa sheria kwa Vyama vya Kitaifa vilivyoyakubali. Vyama vya Kitaifa vilivyo chini ya sheria ya Itifaki ya sasa na marekebisho ya awali ambayo yamekubaliwa.

Kifungu cha 19

- 1) Chama cha Kitaifa kinaweza kukataa Itifaki ya sasa wakati wowote kwa kuandika na kumjulisha Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa. Shutuma zitachukua miezi sita kukubaliwa baada ya tarehe ile ya kumjulisha Katibu Mkuu.
- 2) Shutuma zitakuwa bila ubaguzi na kuendeleza maombi kulingana na Itifaki ya sasa na kwa mawasiliano yoyote yatakayowasilishwa chini ya kifungu cha 2 au uchunguzi ulioanzishwa chini ya kifungu cha 8 kabla ya tarehe hiyo ya shutuma.

Kifungu cha 20

Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa atayaarifu Mataifa yote kuhusu:

- a) Sahihi, uidhinishaji na uthibitishaji chini ya Itifaki ya sasa;
- b) Tarehe ya Itifaki ya sasa ilipoanza kutumiwa na marekebisho yoyote ikiwa yatakuwepo chini ya kifungu cha 18.
- c) Shutuma zozote chini ya kifungu cha 19.

Kifungu cha 21

- 1) Itifaki ya sasa ambayo ina makala ya asili katika lugha ya kiarabu, kichina, kiingereza, kifaransa, kirusi na kihspania itahifadhiwa katika nyaraka za Umoja wa Mataifa.
- 2) Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa atapeleka nakala za Itifaki ya sasa zilizoidhinishwa kwa Mataifa yote yaliyotajwa katika kifungu cha 25 cha Kongamano.